## TAARIFA KWA UMMA

## MAADHIMISHO YA WIKI YA FAMASI KITAIFA TAREHE 10 HADI 16 JUNI, 2022

**Ndugu Wananchi**, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai hadi leo tunapoadhimisha Wiki ya Famasi Kitaifa.

**Ndugu Wananchi,** napenda kuwajulisha kuwa, wanataaluma wa kada ya famasi nchini huadhimisha **Wiki ya Famasi Kitaifa tarehe 10 hadi 16 Juni** kila mwaka, sambamba na **Siku ya Famasi kwa Nchi za Jumuiya ya Madola (COMMONWEALTH PHARMACY DAY)** ambayo huadhimishwa tarehe **16 Juni.** Kauli Mbiu ya mwaka huu inasema ***"Kuwa na Mustakabali wa Pamoja: Kwa kuimarisha Ushirikiano, Kuongeza Ubunifu na Kuleta Mabadiliko katika Huduma za Dawa".***

Katika wiki hii, wakati wanataaluma hawa wakiendelea kutoa elimu na huduma za dawa nchini, (katika vituo vya Umma na binafsi), nitumie nafasi hii kwanza kuwashukuru wafamasia, fundi dawa sanifu na fundi dawa wasaidizi kote nchini kwa kuendelea kufanya kazi bega kwa bega na wataalamu wengine wa afya, wakiwemo madaktari na wauguzi. Serikali kupitia Wizara ya Afya inatambua mchango wa taaluma hii na tutaendelea kuhakikisha kuwa, huduma za dawa na vifaa tiba zinaboreshwa na kupatikana muda wote kwa wananchi hususani wa maeneo ya pembezoni.

kadhaa yanayohitaji kuboreshwa ili kuhakikisha ubora wa huduma za dawa unaendelea kuwa mzuri na wa uhakika siku zote. Ninawataka wanataaluma hawa kuzingatia uwajibikaji, uadilifu, weledi na kuongeza ubunifu ili tuweze kuboresha upatikanaji wa huduma za dawa nchini ambazo ni salama, zenye ufanisi na kwa gharama nafuu.

**Ndugu Wananchi,** taarifa zinaonesha kwamba kumekuwa na ukiukwaji wa sheria katika uendeshaji wa huduma za dawa kwenye maduka ya dawa. Kwa kuzingatia athari zinazoambatana na ufunguaji holela wa maduka ya dawa nchini pamoja na uuzaji holela wa dawa kwa wananchi ikijumuisha usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa, gharama za matibabu kuwa juu na wagonjwa kukaa muda mrefu wodini hivyo kupelekea kupungua kwa nguvu kazi, ninaelekeza vyombo husika hususani Baraza la Famasi na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) kuendelea kuchukua hatua kwa wale wote wanaofanya biashara hii kwa udanganyifu bila kufuata utaratibu.

Aidha, natoa wito kwa wanataaluma wote wa famasi nchini kuendelea kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo katika kutoa huduma za dawa hususani **Kutouza Dawa za Cheti (Prescription medicine) kiholela** kwani ni chanzo cha usugu wa dawa jambo linalotuletea changamoto nyingi za kiafya.

Nawakumbusha wananchi kuwa **Dawa ni Sumu** na hivyo ni vema kuepuka matumizi holela ya dawa bila kupata maelekezo au ushauri wa wataalamu.

Ummy A. Mwalimu (Mb)

**WAZIRI WA AFYA**

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa